
# Hebu na Tuhesabu nyumbani!





Tumia vidokezo hivi vya kusisimua na kiuhalisia kusaidia kutambua, kuchunguza na kuzungumzia hisabati kila siku.

**Vifuatavyo ni baadhi ya vidokezo vya kukusaidia kuanza pamoja na mtoto wako:**

- Wakati wa kutayarisha maakuli ya mchana, zungumza namna unavyoweza kuikata sandiwichi kwa vipande nusu, robo, miraba na mistatili. Unavyo vipande vingapi sasa?








- Pika pamoja! Pima viungo, na wakati mwingine, zungumzia halijoto.

- Tumia muda wa kuoga ili kuchezea na vipimo husika kwa kutumia vikombe vilivyojazwa maji. Ni wanasesere wapi wanazama? Ni wanasesere wapi wanaelea?






**Tambua, chunguza na zungumzia hisabati katika maisha ya kila siku!**

thesmithfamily.com.au

The Smith Family
Learn today, change tomorrow.


# Hebu na Tuhesabu nyumbani!




## Njia za kusisimua zaidi za kuchunguza hisabati nyumbani.

- Mwombe mtoto wako kukusaidia na ufuaji. Panga soksi katika makundimakundi, tambua ruwaza husika.







- Tumia utepe wa kupimia ili kupata urefu wa mtoto. Ni nani ndiye mrefu zaidi katika familia yako? Ni nani ndiye mdogo zaidi?



- Kwenye shamba, ni nini unachoweza kupata? Tambua na chezea maumbo, ukubwa na uzani.



- Chezea mabao au matofali na zungumzia ukubwa, maumbo na ruwaza.

Swahili

**Tambua, chunguza na zungumzia hisabati katika maisha ya kila siku!**

thesmithfamily.com.au

The Smith Family
Learn today, change tomorrow.

# Hebu na Tuhesabu hapa na pale!

Tumia vidokezo hivi vya kusisimua na kiuhalisia kusaidia kutambua, kuchunguza na kuzungumzia hisabati kila siku.

**Vifuatavyo ni baadhi ya vidokezo vya kukusaidia kuanza pamoja na mtoto wako:**

- Cheza nje kwa kutumia maji au changarawe. Tumia vipimo au mikebe ya kupima iliyo na ukubwa tofauti.





- Kule bustanini, cheza kwa kutumia urefu, kimo, umbali, maumbo. Unaweza kupata mraba? Duara?

- Ndani ya gari, tambua na zungumzia kasi na umbali. Umbali upi? Kasi gani? Urefu gani?




Swahili

**Tambua, chunguza na zungumzia hisabati katika maisha ya kila siku!**

thesmithfamily.com.au

The Smith Family
Learn today, change tomorrow.


# Hebu na Tuhesabu hapa na pale!

## Njia za kusisimua zaidi za kuchunguza hisabati nje ya nyumbani.

- Tambua hisabati kwenye dukakuu. Tumia vipimo ili kuchunguza uzani tofauti, zungumzia ukubwa, rangi.


  Je unaweza kupata matofaha mekundu makubwa 2? Gani ndio zito zaidi: tofaha au chungwa.

  Ni nini kimo kwenye toroli yako? Tenganisha vifaa kwa makundi kwa kutumia ukubwa, rangi, umbo.





- Hesabu hatua zako. Kisia ni hatua ngapi hadi kufikia…?




Swahili

**Tambua, chunguza na zungumzia hisabati katika maisha ya kila siku!**

thesmithfamily.com.au

The Smith Family
Learn today, change tomorrow.